



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA HABARI UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO
BODI YA FILAMU TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

Bodi ya Filamu Tanzania ikiwa ni moja ya Taasisi za Serikali inayosimamiwa na Sheria Na. 4 ya Filamu na Michezo ya Kuigiza ya mwaka 1976 pamoja na Kanuni za Sheria hiyo za mwaka 2020, inawajulisha Wadau wote wanaojihusisha na shughuli zote za Filamu na Michezo ya Kuigiza, kuwa imesogeza mbele tarehe ya kuwasilisha maoni ya marekebisho ya Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza za mwaka 2020 zilizotolewa kwenye gazeti la Serikali namba 488 la mwaka 2020. Awali ilikuwa mwishoni mwa Februari, lakini kutokana na maombi ya Wadau kupitia Shirikisho, umeongezwa mwezi mmoja mpaka tarehe 30 Machi, 2021 ndiyo itakuwa mwisho wa kupokea maoni hayo.

Kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo maombi ya Wadau, ilionekana kuna haja/ uhitaji wa kufanyia maboresho Kanuni hizo, hivyo mdau wa Filamu na Michezo ya Kuigiza ambaye anadhani kuna eneo katika Kanuni hizo linahitaji maboresho, anatakiwa kuwasilisha kwa maandishi kwa Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania kwa njia ya jedwali kama ifuatavyo: -

Na.	NAMBA YA KANUNI	JINSI INAVYOSOMEKA	MAREKEBISHO YANAYOPENDEKEZWA

Baada ya kuandika maoni hayo, mdau anaweza kutuma kwa njia ya **PDF** kupitia barua pepe za Bodi (filmboard@habari.go.tz au ceo.filmboard@habari.go.tz).

Aidha, njia nyingine ya kuwasilisha maoni ni kwenda ofisi za Bodi ya Filamu zilizopo Barabara ya Kivukoni, jengo la Utumishi, jijini Dar es Salaam.

Kwa mawasiliano zaidi tafadhali wasiliana na Bodi ya Filamu Tanzania kwa namba; +255 22 2121920.

Imetolewa na;

Bodi ya Filamu Tanzania.